

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

JULAI/AGOSTI 2013

MUDA: SAA 2½

TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA UPILI ZA WILAYA YA NAKURU

Maandalizi kwa Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Muda: Saa 2 ½

Maagizo

- (a) *Jibu maswali manne pekee.*
- (b) *Swali la kwanza ni la lazima.*
- (c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Riwaya, Tamthlia, Ushairi na Hadithi fupi.*
- (d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
- (e) *Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.*
- (f) *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

© 2013 TATHMINI YA PAMOJA SHULE ZA UPILI WILAYA YA
NAKURU

MAANDALIZI KWA CHETI CHA SHULE ZA UPILI KENYA ,

2013 KISWAHILI Karatasi ya 3

FASIHI

Fungua ukurasa

SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI.

1. (a) Maigizo ni nini katika Fasihi Simulizi? (alama 2)
- (b) Taja makundi mawili ya maigizo. (alama 2)
- (c) Bainisha malengo matatu ya kufanya maigizo katika Fasihi Simulizi. (alama 6)
- (d) Eleza sifa tano za maigizo. (alama 10)

SEHEMU B: RIWAYA

Said A. Mohamed: Utengano.

Jibu swali la 2 au la 3.

2. “Katu hatosahau kosa lake. Dunia imemfunza mengi, mengi yamemkuta. . .”
 - (a) Eleza muktadha wa kauli hii. (alama 4)
 - (b) Fafanua makosa manne aliyoafanya mrejelewa ambayo yalichangia kuanguka kwake. (alama 16)
3. Eleza jinsi mwandishi wa riwaya ya Utengano alivyoshughulikia Ukosefu wa maadili mionganini mwa viongozi. (alama 20)

SEHEMU C: TAMTHLIA

Timothy M. Arege: Mstahiki Meya:

Jibu swali la 4 au 5

4. Usishangae mmetuchagua nyinyi. Kama hujui viongozi ni picha ya umma uliowachagua.
 - (a) Eleza muktadha wa kauli hii. (alama 4)
 - (b) Taja sifa nne za mzungumzaji. (alama 4)
 - (c) Huku ukirejelea tamthlia ya Mstahiki Meya, eleza mbinu tofauti ambazo zinatumwi na viongozi katika kujidumisha mamlakani. (alama 12)
5. Kwa kurejelea tamthlia ya Mstahiki Meya, onyesha jinsi mwandishi amefaulu katika matumizi ya mbinu hizi za lugha:
 - a) Kinaya. (alama 10)
 - b) Jazanda (alama 10)

SEHEMU D: USHAIRI.

Jibu swali la 6 au 7.

6. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Viumbe wa siku hizi, tamaa zimewashika,
Mtu japo ana kazi, ya cheo na madaraka,
Atafanya uchafuzi, kuharibu mamlaka,
Apoteze uazizi, Mungu alomtunuka,
Cheo na kupanda ngazi, awe ni mwenye kushuka.
Na ajili ya kutenda, hutongewa ni tamaa,
Tamaa zimemshinda, moyoni zimemjaa,
Akitaka kujilinda, roho yamwambia twaa,

Heshima akaivunda, kwa kutenda yasofaa
Jinale akaliponda, akarudi kuduwa.

Tamaa dunia nzima, sasa imeshika zamu,
Sioo kwa wenye kusoma, wala wasiyo elimu,
Watu wamekuwa nyama, kwa kutaka darahimu,
Tarajia ni kuchuma, jingine hawafahamu,
Mara huwa wamezama, na lengo halikutimu.

Haya niliyoyatunga, siyo mambo ya kubuni,
Siku hizi kila janga, hutangazwa radioni,
Kuna wezi wa mapanga, wangiao majumbani,
Wengine hujikonga, kuwadhuru Insani,
Ili wapate faranga, tamaa zao nyoyoni.

Wengine hufanikiwa, bahati ikiwa nzuri,
Wakenda wakachukuwa, kama vyao kwa shuari,
Na kwengine huuawa, wakachimbiwa kaburi,
Wakabaki kufukiwa, pasipo na dua nzuri,
Na yote yasingekuwa, tamaa zimewaghuri.

Nilipofika unasi, natia kaditamati,
Najua mtu hakosi, tamaa kila wakati,
Lakini zisitughasi, zikatupa taslitii,
Na nyendo za Ibilisi, hazikosi tafauti,
Kupata siyo kwa kasi, kupata kuna wakati.

SAID HAMADIL

- (a) Lipe shairi hili kichwa. (alama 2)
- (b) Hili ni shairi la aina gani. Toa sababu. (alama 2)
- (c) Taja madhara manne yanayosababishwa na hamu iliyokithiri. (alama 4)
- (d) Huku ukitoa mifano tambua mbinu mbili za lugha alizotumia mtunzi wa shairi hili. (alama 4)
- (e) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
- (f) Andika ubeti wa 6 kwa lugha nathari. (alama 4)

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Sibabaiki wala sitishiki
Kweli asonacho
Ni hasidi ya mwenecho
Enyi wenye mwao
Bure pumzi mwapoteza
Yagonga mwamba mnoamba

Mahasidi
Zani mwanibwagia
Ja mahoka mwapyora
Mie dhuli mwalonga
Mwalalama eti mie barakala

Kila kuchao
Mie nazidi kutononoka
Rabana nafasi kanijaalia
Yanyoka sasa yangu
Gere mnaona, kazi bure

Usabasi mnonipulizia
Syo marashi katu
Bali kero tups
Kutoteterska ndiyo yangu kinga na ngao
Mola tanisitiri
Mwerrevu hapigani kwa ngumi
Ngomeze na silahaze ni hulkaze

Meli haitishi bahari
Si kitu baiskeli mbele ya gari
Mbao haitishi chuma
Kigoda si ja kochi
Maji moto hayachomi nyumba

Stara menipa Rabi
Huo upofu sina
Nyota ya jaha naiola kinishukia
Kutoka janibu za matlai
Kuko huko naelekea
Kwa subirà na idili mzo mzo
Kwa ghera na hamasa ghaya

Mie si hawafu
Chatu hanibabaishi, sembuse kijoka!
Bafe si kitu kwangu mie, seuze lumbwi!
Swila na pili huwahilikisha, kaifa mjusi kafiri!
Ligaye mamba siogopi, iweje niogope mburukenge!

- (a) Eleza dhamira ya shairi hili. (alama 2)
- (b) Huku ukitoa mifano, taja aina mbili za idhini ya utunzi wa mashairi alizotumia mshairi. (alama 4)
- (c) Taja mambo matatu yanayomkumba msimulizi kulingana na shairi hili. (alama 6)
- (d) Mshairi anamanisha nini anaposema
 - (i) Zani mwanibwagia.
 - (ii) Usabasi mnonipulizia. (alama 4)
- (e) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (alama 4)

SEHEMU E: HADITHI FUPI

8. Bainisha na ueleze mifano kumi ya jazanda katika hadithi ya Kikaza. (alama 20)

Huu ndio ukurasa wa mwisho uliopigwa chapa.